# KISWAHILI LUGHA

# DARASA LA NNE

# 2015

**AVAILABLE ONLINE AT:**

Schools Net Kenya Consultancy

**P.O. Box 8076 – 00200 Nairobi, Kenya | Tel: +254202319748**

**E-mail: infosnkenya@gmail.com | www.schoolsnetkenya.com**

## KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujaze nafasi 1 - 10 zilizoachwa wazi.***

Hadithi hadithi! Hapo zamani ____1____ kale, paliondokea mwanamke mmoja ____2____ aliyeumbwa ____3____. Msichana ____4____ aliitwa Katerina. Msichana huyu alilelewa ____5____ kutunzwa vizuri na wazazi ____6____ hadi mama ____7____ umri ____8____ kuolewa.

Watu ____9____ viwete, vilema, matajiri na ____10____ walifika ili kuomba kumuoa ____11____ pamoja na wazazi wake walikataa watu hao ____12____. Nia yao kubwa ____13____ Katerina ____14____ na mkulima. Furaha kubwa ilijaa nyumba yao, alipoolewa na mkulima ____15____.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | za | ya | cha | kwa |
| 2. | akaumbwa | pamoja | mmoja | mmonja |
| 3. | hajaumbika | akaumbika | akaundwa | akaumbikiwa |
| 4. | ule | huo | hii | huyu |
| 5. | na | kwa | pa | wa |
| 6. | chake | zake | yake | wake |
| 7. | anapofikisha | amefikisha | alipofikisha | atafikisha |
| 8. | ya | wa | cha | za |
| 9. | bali | mbalibali | mbali | mbalimbali |
| 10. | maskini | maskani | masikini | mashakani |
| 11. | mimi | wewe | yeye | nyinyi |
| 12. | kote | wote | yote | lote |
| 13. | unakuwa | ilikuwa | imekuwa | itakuwa |
| 14. | aoe | auzwe | auze | aolewe |
| 15. | hodari | mvivu | mchoyo | mbaya |

***Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu sw...***

***...aswali***

Iwapo ungependa kujikinga r...
aina mbalimbali ya maradhi ambay... ...ni" ni
kipindupindu na homa ya matur...

Ili kujikinga na mar...
magonjwa kutokana n...
malaria. Ugonjwa... ...ngo. Hamisi alikunywa maji kwa

Hata h... ...umia

Yeyote ak...

41. ...


A. chano
B. bilauri
C. kinu
D. mchi

**18.** Tumia neno sawa kukamilisha sentensi hii.
Samaki _____ majini.
A. zilikufa
B. ilikufa
C. inakufa
D. alikufa

**19.** Jaza pengo kwa kutumia neno lifaalo
Mkulima _______ mimea maji.
A. alinyunyizia
B. alifyeka
C. alipanda
D. alipalilia

**20.** Andika wingi wa: Mimi huenda shuleni.
A. Wao huenda shuleni.
B. Nyinyi huenda shuleni.
C. Sisi huenda shuleni.
D. Yeye huenda shuleni.

**21.** Umbo hili huitwa



A. mche mraba
B. pia
C. mstatili
D. mche mstatili

**22.** Tegua kitendawili. Huko ng'o na kule ng'o
A. mwezi  B. usiku
C. mweusi  D. giza

**23.** Ugonjwa unaosababishwa na umbu ni
A. malaria
B. malale
C. mbung'o
D. nzi

**24.** Kanusha. Tunakula chakula.
A. Hatukukula chakula.
B. Hatuli chakula.
C. Hukuli chakula.
D. Hatujakula chakula.

**25.** Akisami $\frac{1}{2}$ huitwa
A. robo
B. thuluthi
C. nusu
D. kamili

**26.** Kamilisha methali. Pole pole ndio
A. mwendwa
B. adabu
C. ukweli
D. mwendo

**27.** Ni nini kinyume cha "anika"?
A. Vua
B. Anua
C. Inua
D. Anikisha

**28.** Mwanafunzi aliyeadhibiwa ni
A. wangu
B. yangu
C. mwetu
D. yetu

**29.** Wingi wa kalamu ni
A. makalamu
B. tulamu
C. kalamu
D. vilamu

**30.** Ni gani si ndege?
A. Mwewe
B. Bundi
C. Kunguru
D. Popo

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya* **31- 40.**

Kwa kweli binadamu ni kiumbe aliyeumbwa na mwenyezi Mungu kwa njia ya ajabu sana. Kila binadamu ana viungo tofauti kama vile macho, mikono, miguu au hata mikono.

Akili ni nywele na kila mtu ana zake. Akili humsaidia mtu kufikiria na kujua kati ya jambo jema na baya. Karina alikuwa mwanafunzi wa darasa la nne katika shule ya Mbalambala karibu na mji wa Ndarumi.

Siku moja alipokuwa anaelekea nyumbani kutoka shuleni, alikutana na mtu asiyemjua. Alipomsalimia salamu za alasiri akichekacheka, alimwomba aandamane naye. Mtu huyu alimuahidi kwamba angemununulia soda wafikapo dukani.

Kwa hekima, Karina alikataa katakata. Kwa wakati huu, alimkumbuka rafikiye Mwebia baada ya kudanganywa na mtu asiyemfahamu alibakwa na mwishowe kuuawa. Pia Karina alikumbuka mawaidha ya mwalimu wake kuwa usikaribie mtu usiyemjua wala kuchukua chochote chake.

Alikimbia na kumuacha. Alifika nyumbani na kumweleza mama yake mambo yote na mama akamkumbusha na kumshauri kujiweka mbali na watu asiowajua.

Hekima yake ilimfanya apendwe zaidi na wazazi na walimu wake shuleni. Alifanya vizuri kwa mitihani yake yote na akajiunga na sekondari. Kisha baadaye akawa mwanariadha hodari na basi akajiunga na timu ya riadha.

**31.** Ni kiungo gani cha mwili hakijatajwa?
A. Macho B. Miguu
C. Mabega D. Masikio

**32.** Karina alikuwa mwanafunzi katika shule gani?
A. Ya Ndarumi
B. Mbalambala
C. Njueni
D. Nkungani

**33.** Rafikiye Karina aliitwaje?
A. Hekima
B. Mwebia
C. Harun
D. Mbalambala

**34.** Karina aliahidiwa kununuliwa:-
A. Mkate B. Andazi
C. Soda D. Peremende

**35.** Kulingana na taarifa, Karina alikuwa mwanafunzi;
A. mwenye hekima
B. mtundu
C. mjinga
D. dhaifu

**36.** Katika shule, Karina alijiunga na timu ya
A. kandanda
B. riadha
C. raga
D. kuogelea

**37.** Si kweli kusema kuwa Karina
A. alipendwa na walimu wake.
B. alipita mtihani.
C. alikuwa mtoto mwenye heshima.
D. alianguka mitihani yake.

**38.** Karina alifanya nini baada ya kukumbuka ushauri wa wazazi wake?
A. Alienda dukani na mtu asiyejua.
B. Alitoroka
C. Alilia
D. Alipiga ukemi

**39.** Karina alikuwa wa darasa la
A. nane B. saba
C. tano D. nne

**40.** Kichwa kinachofaa hadithi hii ni
A. Mwacha mila
B. Elimu
C. Shuleni bila heshima
D. Hekima

*Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu swali la 41 - 50*

Iwapo ungependa kujikinga na maradhi mbalimbali hapa nchini ni lazima yeyote awe safi. Kuna aina mbalimbali ya maradhi ambayo huambukizwa na wadudu wa uchafu. Mfano ni nzi ambao huambukiza kipindupindu na homa ya matumbo. Magonjwa haya huharisha pia kutapisha.

Ili kujikinga na maradhi haya ni <u>sharti</u> kila mmoja awe safi. Wadudu wengine ambao huambukiza magonjwa kutokana na uchafu ni chawa na kunguni. Mbu pia huambukiza magonjwa. Ugonjwa huu ni malaria. Ugonjwa huu huua.

Hata hivyo kuna magonjwa mengine mengi yasiyo ya uchafu. Mfano; kifafa, upele na mafua. Yeyote akiugua anastahili apelekwe hospitalini ili atibiwe. Kumbuka maradhi huua.

**41.** Jina jingine la maradhi ni
A. malale
B. ugonjwa
C. kichocho
D. kifafa

**42.** Ni ugonjwa gani unaoambukizwa na mbu?
A. Malale
B. Kifafa
C. Kifaduro
D. Malaria

**43.** Nzi huambukiza ugonjwa upi?
A. Kipindupindu
B. Upele
C. Mafua
D. Ukimwi

**44.** Ili kujikinga na magonjwa ni lazima kila mmoja awe ______
A. Mchafu
B. Muungwana
C. Safi
D. Mwangalifu

**45.** Neno sharti limepigiwa mstari. Maana yake ni
A. sharti
B. lazima
C. vyema
D. uzuri

**46.** Ni sentensi ipi isiyosahihi?
A. mtoto msafi haugui
B. mtoto msafi anaugua
C. mtoto msafi hauguangi
D. mtoto safi haugui

**47.** Ni mahali gani mtu hupelekwa kutibiwa anapougua?
A. Hospitali
B. Shuleni
C. Nyumbani
D. Kanisani

**48.** Ni ugonjwa gani haujatajwa kwenye ufahamu?
A. Kifafa
B. Pepopunda
C. Kuendesha
D. Ukimwi

**49.** Ni wadudu gani hawajatajwa katika ufahamu huu?
A. Nzi
B. Chawa
C. Kombamwiko
D. Kunguni

**50.** Ni kichwa gani kifaacho ufahamu huu?
A. Uchafu
B. Usafi
C. Elimu
D. Maradhi